# Ugonjwa Afya na Uponyaji



KAZI ZA WARSHA

## Kuhudumia Afya ya Jamii yetu

Katika kukuza ufahamu wetu, kutoa huduma na msaada kwa wale wanaohitaji.

**Mpango wa muungano wa SCWA**

Toleo 2021–01b
hakimiliki © SCWA — haki zote zimehifadhiwa

info@stop–cwa.org

*translator for Kiswahili edition:*
*Marco Methuselah*

Edition 2021–01b

# Warsha ya Siku Moja

## UGONJWA, AFYA, NA UPONYAJI

**Kusudi Kuu la Mfululizo wa mafunzo:** Raslimali zote za mafunzo katika ukweli wa mambo zinalenga kutoa mwitikio wa maana katika tatizo la ushukiwaji wa uchawi unaofanywa dhidi ya watoto na wenye mtazamo wa kuleta mabadiriko katika utamaduni na mwenendo katika jamii za kawaida.

**Lengo la warsha hii:** Mwishoni mwa warsha hii washiriki watakuwa wameelewa kuwa ugonjwa na mauti sio tu vinanasibishwa na uchawi na hali ya kutafuta uponyaji kwa njia ya matendo ya uharibifu unaopaswa kuepukika.

---

### Kabla ya Warsha

Kusanyikeni na kuandaa yafuatayo:

- Vifaa — Flipchati, kalamu za kuwekea alama, karatasi, kalamu, gundi ya mkanda.
- Nakala za makala ya Biblia, zilizochapwa katika karatasi.
- Nakala za maswali ya mijadala ya vikundi (zitakazotolewa kwa kila kundi kabla ya kazi husika).

Unapaswa kuhakikisha unatambua wanandoa wawili (huenda wachungaji na wake zao) wanaoweza kujadiri na kuombea mahitaji ya washiriki yaliyoletwa mbele za warsha yanayohusu kupoteza ndugu au jamaa. Kazi hii hasa inahusu zoezi la 6.

**Angalizo kwa mwezeshaji**: katika mazoezi, inafikiriwa kuwa mwezeshaji atakisoma kisa kama kilivyojitokeza. Hata hivyo, akipenda, wengine wanaweza kusoma au wasaidizi wanaweza kuvisoma visa hivyo (kusoma mazungumzo, na msimuliaji asome sehemu za kisa zilizobakia). Huenda ni rahisi zaidi kufanya hivi kutumia wasaidizi watakaokuwa wameandaa mapema, ingawa inaweza kufanyika pamoja na washiriki endapo wapo tayari kuhusishwa katika njia hiyo na kama wanapenda kusoma katika notisi.

### Na Hatimaye ...

Kwa washiriki kama kumbu kumbu ya mahudhurio yao ya warsha, utahitaji:

- Vyeti vya Washiriki— hivi vitahitaji kuchapwa, kuwa na majina ya walihudhuria, na kusainiwa na mwezeshaji. Mfano wa cheti umetolewa pamoja na rasilimali ya somo hili.

---

# Kufungua (sio zaidi ya dakika 30)

## Maombi na kuabudu

Mkaribishe mshiriki kuongoza wimbo wa kuabudu.

**Muombe mshiriki mwingine** kuomba na kuikabidhi siku kwa Mungu, na kumuomba Mungu kuongea na kila mmoja katika mafundisho.

## Utangulizi

Ikiwa mafunzo ya *Ugonjwa, Afya, na Uponyaji* yatatumika kama somo lililosimama peke yake, kuliko kuwa *Kiini cha Jambo*, basi jitambulishe mwenyewe na waulize washiriki wajitambulishe wenyewe kwa kifupi.

# Zoezi 1: Utangulizi (dakika 15)

**Lengo** — Kuwafanya washiriki kukumbuka uzoefu wa ugonjwa; kutambua kuwa ugonjwa hutokea kwetu sisi wote; na kuonesha jinsi mtu alivyoonesha upendo na kujari na msaada ulioleta hali ya usalama.

## Kuandaa muktadha

**Tambulisha somo kama ifuatavyo**:

> Ugonjwa na mauti ni hali halisi ya kila siku katika jamii zetu. Leo, tutakwenda kuangalia jinsi jamii zetu zinavyojibu maswali kuhusu ugonjwa, afya, na uponyaji, na kuhusu Biblia inatufundisha nini kuhusu hayo yote. Kisha tutafikiria namna tunavyoweza kujenga mwitikio wa fikra yakinifu na kuepuka maumivu zaidi na mateso katika jamii zetu yatokanayo na fikra hasi au miitikio hasi.

**Waulize washiriki** kuinua mikono yao endapo wameshawahi kuwa wagonjwa mwaka mmoja uliopita. Kisha uliza kama watu watatu ambao wako tayari kushirikisha kitu ambacho hakikuwaendea vizuri. **Waruhusu washirikishe** kwa kifupi.

**Kisha waulize** washiriki wote kufikiri kuhusu kipindi ambacho waliwahi kuwa wagonjwa sana maishani mwao. Waombe wafikirie kuhusu mtu aliyewajari na kuwaonesha msaada wa upendo na namna msaada huo ulivyo wasaidia kupona.

**Waalike washiriki wawili** ambao wako tayari kushirikisha kuhusu watu waliowasaidia kupata nafuu. Walisaidiwa kuhusu nini hadi kufikia kupata nafuu au kupona kabisa? Walifanya nini ili kuwasaidia kupata unafuu na kujisikia kusaidiwa?

**Elezea yafuatayo:**

Kupenda na kujari na kutoa msaada kunaweza kumfanya mgonjwa kujisikia vizuri. Kama wafuasi wa Kristo, tumeitwa kutoa msaada kama huo kwa wanafamilia wetu na jamii zetu waliowagonjwa na walio katika mazingira magumu.

Kama Luka 6:31 inavyosema . . .

> *Wafanyie wengine ambavyo ungependa wakufanyie wewe*

# Zoezi 2: Matukio na Mijadara (dakika 40)

**Lengo** — Kulitambulisha somo na kuangalia zaidi kwa mapana kuanza kutazama miitikio ya jamii katika ugonjwa, majeruhi, na mauti.

**Kuandaa washiriki** katika vikundi vidogo vidogo, na kuliomba kila kundi kuchagua mwandishi kuandika kumbu kumbu za mijadara na miitikio yake. Mpatie mwandishi kipande cha karatasi pamoja na kalamu ya kuwekea alama. Pia mwandishi atashirikisha miitikio hii kwa washiriki wengine baada ya mjadara.

**Wapatie kila kundi tukio moja** kulijadiri na waulize wafikirie maswali yafuatayo:

- Unafikiri kinatokea nini?
- Unafikiri kitu gani kilisababibisha hali hiyo inayoelezewa?
- Unafikiri familia na marafiki wafanye nini?
- Unafikiri ni kitu gani hasa kinaweza kutokea kwa aliyejeruhiwa au kuugua? **Ruhusu dakika 10** kwa kundi kujadiri tukio walilopewa.

## Tukio 1

Erenesti ni mwanaume wa kiaka hamsini. Alikuwa anawahi mkutano akivuka barabara katika eneo la kona, na pikipiki ikamgonga. Erenesti alirushwa hewani na kutua chini katika barabara. Hakujielewa maana aligonga kichwa chake chini. Kichwa chake, mikono na miguu ilivurutwa na kuvuja damu.

## Tukio 2

Yosia ana miaka sitini na kawaida yuko imara na afya njema. Kwa Juma lililopita amekuwa akijisikia vibaya. Ana homa na maumivu mwilini. Ana maumivu katika viungo vya mwili wake. Anasema hataki kula kwasababu anahisi kutapika, lakini ana kiu sana.

## Tukio 3

Silvia ana umri wa miaka minne lakini anaonekana mdogo zaidi. Ana uzito mdogo, utapia mlo, na ni dhaifu sana. Hawezi kusimama tena au kukaa bali yeye hulala katika godoro

lake kimya akiwa amefumba macho. Kupumua kwake ni dhaifu, na hajibu mama yake anapomuongelesha.

Baada ya dakika 10, **muombe mwandishi ashirikishe** mwitikio wa kikundi kwa kila mmoja.

**Kisha waulize vikundi kujadiri** maswali yafuatayo**:**

- Kuna imani gani katika jamii zetu kuhusu ugonjwa na uponyaji?
- Ni imani zipi zinazoamua kuhusu sababu za ugonjwa?
- Tunajikingaje sisi wenyewe dhidi ya magonjwa?
- Tunaitikiaje kwenye magonjwa? Hutokea nini mtu akiugua katika jamii yetu?
- Huwa tunatafuta wapi uponyaji? Huwa tunamtafuta nani kushauri? **Baada ya dakika 20,** muombe msemaji wa kikundi kutoka kila kundi kutaarifu mwitikio (majibu) ya kikundi kwa kila mshiriki.

**Yaandike majibu** katika karatasi ya flip chati, na kisha ibandike hiyo flip chati ukutani. Elezea kuwa tutarejea tane katika haya majibu baadae.

## Zoezi 3: Kisa na Mjadara (dakika 20)

**Lengo** — Kukitambulisha kisa hiki na kuyachunguza maudhui yanayohusiana na magonjwa na uponyaji.

### Kisa chetu kinaanza . . .

**Wasomee kwa sauti washiriki,** taratibu na kwa kueleweka, kisa kifuatacho:

> *Samweli na mke wake Estha wanaishi na mama yao mzee, Yunisi, na watoto wao Paulo (umri wa miaka 10) na Raheli (miaka 8). Pia wanaishi na Gideoni (umri wa miaka 12), ambaye ni mwana wa Samweli kutoka katika mahusiano ya awali. Samweli ana fanya kibarua, na Estha huuza nyanya kando kando ya barabara. Asubuhi moja, Estha aliamka anaumwa. Alikuwa anaumwa kichwa sana, homa, kuharisha, na kichefu chefu. Alikuwa hajisikii vizuri kiasi cha kushindwa kula, aliendelea kujisikia dhaifu siku hadi siku kwa siku chache zilizofuata.*

**Kisimamishe kisa hapa**

Waulize washiriki wapendekeze kinachojiri. Ruhusu vipengele vine au vitano vipendekezwe na viandike katika flip chati.

Kisha **wapange wahiriki katika makundi** ya watu 6 hadi 8.

**Waombe wajadiri maswali yafuatayo katika makundi yao**:

- Ni yapi katika matokeo yaliyopendekezwa yanafanana na ugonjwa wa Estha hasa katika jamii yetu?
  - Ni nini matokeo ya kila matokeo yaliyopendekezwa yanaweza kuwa: Katika familia moja moja?

  - Katika familia kwa ujumla?
  - Katika jamii katika ukubwa wake?
- Yangepatikana matokeo gani yakinifu zaidi au matokeo hasi zaidi?

**Angalizo kwa muwezeshaji:** Maswali haya yanaweza kuandikwa katika karatasi ya flip chati na kubandikwa katika ukuta mwanzoni mwa zoezi. Vinginevyo, maswali yanaweza kuandikwa katika vipande vidogo vya karatasi vitakavyogawiwa kwa washiriki wote.

**Liulize kila kundi** kuchagua msemaji ili kutoa mrejesho wa majibu ya maswali baada ya kila mjadara.

**Baada ya dakika 10**, muulize msemaji kutoka kila kundi kutoa mrejesho wa vipengele kwa kila mshiriki wa kila kundi.

**Karibisha miitikio** kutoka kila mmoja na ongoza mjadara ili kugundua:

- Ni hatua gani zitakazofuata zitamaanisha kuwa watu wote katika familia walikuwa wamelindwa na kupewa uangalizi?
- Ni hatua gani zitakazofuata zitahakikisha kuwa familia zinabakia katika umoja?
- Ni hatua gani zaidi zingeweza kukuza imani dufu na kujari katika jamii?

## Zoezi 4: Tafakari ya Biblia (dakika 45)

**Lengo** — Kuangalia Biblia inatuambia nini kuhusu ugonjwa, afya, na uponyaji.

**Bandika vipande vitano vya karatasi ya flip chati ukutani,** kila moja ikiwa na maelezo yafuatayo juu yake, kukiwa na nafasi chini yake kwa ajiri ya rejea za Biblia.

**Angalizo kwa mwezeshaji:** maandalizi yanatakiwa yafanyike mapema. Mungu aliwaumba wanadamu. Mungu aliuunda mwili wa mwanadamu, hivyo Mungu anaufahamu vizuri kabisa.

1. Magonjwa na mauti vilimwijia mwanadamu kwasababu Adamu na Eva walitenda dhambi katika Bustani ya Edeni (Mwanzo 3). Magonjwa na mauti havikuwa sehemu ya uumbaji ‘mzuri sana’ wa Mungu alioufanya, lakini vilitokea kwa sababu ya ukaidi na uasi wa Adamu na Eva, na sasa ni sehemu ya maisha ya mwanadamu.

2. Biblia inavichukulia afya na magonjwa katika hali ya ujumla. Inaelezea afya ya mtu mzima na sio tu afya ya mwili. Inarejea katika hisia, kiroho, kifikra, na katika afya ya akili, pamoja na afya ya mwili.

3. Mungu anatawala. Hakuna ugonjwa wala kifo, zaidi ya uwezo Wake. Mungu anaweza kuponya. Lakini huwa hachagui mara zote kuponya, hadi sasa kifo kipo. Wakati mwingine Mungu huruhusu magonjwa na mateso mengine ili kukamilisha kusudi Lake kubwa katika maisha yetu, kutusaidia kukomaa katika tabia na mienendo yetu, kutufundisha kumtegemea Yeye, au kwa sababu zingine ambazo hatuwezi kuzifahamu kikamilifu.

4. Yesu alikuja kuleta tumaini na uponyaji. Kwa sababu yake, matokeo ya uasi wa mwanadamu utakomeshwa, na hapatakuwa na mateso wala mauti tena.
5. Yesu alikuja kuleta tumaini na uponyaji. Kwa sababu yake, siku moja matokeo ya uasi wa mwanadamu utakomeshwa, na hapatakuwa na maumivu wala mauti tena.

**Elezea** kuwa tusikilize baadhi ya aya katika Biblia na kuzilinganisha na maelezo yaliyoko katika flip chati. Baadhi ya maelezo yanatakiwa yakubaliwe na dondoo za maandiko.

**Waombe watu wa kujitolea** ambao wanapenda kusoma aya kutoka katika Biblia. Wagawie karatasi za maandishi yenye aya za Biblia. Endapo hapatakuwa na wenye kujitolea, au hawatoshi, kisha mwezeshaji au msaidizi anaweza kuzisoma hizo aya zote.

**Angalizo kwa mwezeshaji:** vitu hivi vinapaswa kuandaliwa mapema.

## Aya za Biblia

**Isaya 65:17–20**

> *“Maana, nitaumba mbingu mpya nan chi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni. Bali furahini na mshangilie daima, kwa ajiri ya hivi niviumbavyo; maana, tazama, naumba Yerusalemu uwe shangwe, na watu wake wawe furaha. Nami nitaufurahia Yerusalemu nitawaonea shangwe watu wangu; sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, wala sauti ya kuomboleza. Hatakuwepo tena mtoto wa siku chache, wala mzee asiyetimia siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa.*

Aya hizi zinaendana na maelezo 5. Washiriki wakishagundua hili, kisha (mwezeshaji au msaidizi wake) wataiandika ‘Isaya 65:17-20’ mbele ya maelezo 5, ambayo yako katika kipande cha karatasi ukutani.

**Warumi 5:12**

> *Kwahiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo, mauti ikawafikia watu wote kwasababu wote wamefanya dhambi.*

Aya hii inaendana na maelezo 2. Washiriki wakishagundua hivi, andika Warumi 5:12’ mbele ya maelezo 2, ambayo iko ukutani.

**Zaburi 119:71**

> *“Ilikuwa vyema kwangu kuwa niliteswa, nipate kujifunza amri zako.”*

Aya hii inaendana na maelezo 4. Washiriki watakapogundua hili, kisha iandike Zaburi 119:71’ mbele ya maelezo 4, amabyo yako ukutani.

**Zaburi 139:13-16**

> *"Maana wewe ndiwe uliyeniumba utu wangu wa ndani, uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakusifu kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana. Mifupa yangu haikusitirika kwako, nilipoungwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi pande za chini ya nchi. Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; chuoni mwako ziliandikwa zote pia, siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado."*

Aya hizi zinaendana na maelezo 1. Washiriki wakigundua hili, andika Zaburi 139:13-16 mbele ya maelezo 1, yaliyoko ukutani.

**Hosea 11:3**

> *"Nitaziponya njia zao na kuwapenda bure, kwa kuwa hasira yangu imeondoka kwao."*

Hii inaendana na maelezo 3. Washiriki watakapotambua hili, andika Hosea 11:3' mbele ya maelezo 3, yaliyoko ukutani.

**Kutoka 15:26**

> *"Mimi ni Bwana, niwaponyae."*

Hii inaendana na maelezo 4. Washiriki watakapotambua hili, kisha andika 'Kutoka 15:26' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**Zaburi 103:2–4**

> *"Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, Naam, wala usizisahau fadhili zake zote. Akusamehe makosa yako yote, akuponye magonjwa yako yote, Aukomboae uhai wako na kaburi, akutiae taji ya fadhili na rehema."*

Aya hii inaendana na maelezo 4. Washiriki watakapogundua hili, andika Zaburi 103:2–4 mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**2 Wafalme 4: 32–35**

> *Basi Elisha alipofika nyumbani, tazama, mtoto amekwisha kufa, amelazwa kitandani pake. Akaingia ndani, akajifungia mlango, yeye na yule mtoto wote wawili, akamwomba BWANA. Akapanda juu ya kitanda, akajilaza juu ya mtoto akaweka kichwa chake juu ya kichwa chake, na macho yake juu ya macho yake, na mikono yake juu ya mikono yake, akajinyoosha juu yake; mwili wake yule mtoto ukaanza kupata joto. Kisha Elisha akarudi, akatembea nyumbani, huko na huko mara moja; akapanda, akajinyoosha juu yake; na yule mtoto akapiga chafya mara saba na kafumbua macho yake.*

Aya hii inaendana na maelezo 4. Endapo washiriki awatagundua hili, andika '2 Wafalme 4:32–35' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**Zaburi 147:3**

> *Mungu huwaponya waliopondeka moyo, na huziganga jeraha zao.*

Aya hii inaendana na maelezo 3. Endapo washiriki watagundua hili, andika Zaburi 147:3' mbele ya maelezo 3, yaliyoko ukutani.

**Isaya 57:1-2**

> *Wenye haki hupotea; wacha Mungu hufa kabla ya wakati wao. Wala hakuna afikiriye ya kuwa mwenye haki ameondolewa asipatikane na mabaya. Yeye huingia katika amani wanapokufa.*

Aya hii inaendana na maelezo 4. Endapo washiriki watagundua hili, kisha andika 'Isaya 57:1–2' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**Elezea** kuwa aya hizi huonesha kuwa ingawa hatutaweza kuelewa kwanini mtu fulani amefariki akiwa kijana au kabla ya wakati, Mungu huona picha kubwa.

**Kumbukumbu la torati 32:39**

> *"Hakuna Mungu zaidi yangu. Naua mimi, nahuisha mimi, ninajeruhi na ninaponya, hakuna wala hakuna awezaye kuokoa katika mkono wangu."*

Aya hii inaendana na maelezo 3. Endapo washiriki watagundua hili, Mwezeshaji au msaidizi wake waandike 'Kumbukumbu la Torati 32:39' mbele ya maelezo 3, yaliyoko ukutani.

**Ufunuo 21:4**

> *"Mungu atawafuta kila chozi katika macho yao. Hapatakuwa na mauti au vilio au maombolezo, au maumivu, maana mambo ya kale yatakuwa yamepita."*

Aya hii inaendana na maelezo 5. Endapo washiriki watagundua hili, kisha andika Ufunuo 21:4' mbele ya maelezo 5, ambayo yapo ukutani.

**Yohana 9:3**

> *"Sio huyu (kipofu) wala wazazi wake hawakutenda dhambi," Yesu akasema, hii imetokea ili kwamba kazi ya Mungu idhihirishe ndani yake."*

Haya yanaendana na maelezo 4. Endapo washiriki watagundua hili, andika 'Yohana 9:3' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**Zaburi 69:20**

> *Laumu (mahusiano yaliyovunjika) imenivunja moyo na kuniacha bila msaada; nilitazamia wa kunihurumia na kunipa faraja wala hapakuwa na mtu hata mmoja.  lakini hapakuwa hata mmoja.*

Aya hii inaendana na maelezo 3. Endapo washiriki watagundua hili, andika 'Zaburi 69:20' mbele ya maelezo 3, yaliyoko ukutani.

**Yeremia 32:27**

> *Mimi ni Bwana Mungu, Mungu wa wote wenye mwili. Je kuna jambo nisiloliweza?*

Aya hii inaendana na maelezo 4. Endapo washiriki watagundua hili, andika 'Yeremia 32:27' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**Mwanzo 1:27**

> *Mungu alimuumba mwanadamu katika mfano wake, mwanaume na mwanamke aliwaumba katika mfano na sura ya Mungu.*

Aya hii inaendana na maelezo 1. Endapo washiriki watagundua hili, andika 'Mwanzo 1:27' mbele ya maelezo 1, yaliyoko ukutani.

**Yakobo 1:2–4**

> *Ndugu zangu Hesabuni kuwa na furaha, mkiangukia katika majaribu mbali mbali, mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa Imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.*

Aya hii inaendana na maelezo 4. Endapo washiriki watagundua hilli, kisha andika 'Yakobo 1:2–4' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**2 Timotheo 4:20 and 1 Timotheo 5:23**

> *"Mimi (mtume Paulo) nilimwacha Trofimo anaumwa huko Mileto*
>
> *"Usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajiri ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara."*

Aya hizi zinaendana na maelezo 4. Endapo washiriki watagundua hili, Mwezeshaji au msaidizi wake aandike '2 Timotheo 4:20 na 1 Timotheo 5:23' mbele ya maelezo 4, yaliyoko ukutani.

**Koleza vipengele** tunavyovifahamu kutoka katika kitabu cha Matendo ya Mitume kuwa Mungu alifanya miujiza ya uponyaji kupitia Paulo (tazama Matendo 14:8-10 na Matendo 28:8), ikiwa ni pamoja na aya zingine), lakini rejea za Timotheo na Trophimo zinaonesha kuwa Mungu hakuchagua kuponya kila wakati, ingawa kuwa Paulo aliwaombea hawa marafiki zake wa karibu.

## Mapitio na Tafakari

**Sasa,** yasome kwa sauti maelekezo matano tena.

Waalike washiriki waungane katika vikundi vyao vidogo na wajadiri kwa dakika 15 wakitumia maswali yafuatayo:

- Kitu gani kinakuamsha kutoka maelezo haya?
- Tunaweza kujifunza nini kutoka katika maelezo hayo?

- Tunawezaje kuyatumia haya kwetu leo?

**Baada ya dakika 15,** muombe msemaji kutoka kila kundi kushirikisha miitikio yao kwa kila mmoja.

**Sisitiza vipengele vifuatavyo**:

- Dhambi hututenganisha sisi na Mungu. Kutengwa na Mungu husababisha matokeo ya ugonjwa na mauti. Kupitia Yesu na kazi zake pale msalabani, wale wanaompenda hurejeshwa katika mahusiano pamoja na Mungu. Lakini hadi sisi Wakristo hatupokei miili isiyoharibika, miili yetu itaendelea kuzeeka na kufa mpaka Yesu Kristo atakaporudi. Magonjwa na mauti ni sehemu ya matakwa ya mwili. Biblia inasema kuwa Wakristo waaminifu wanaweza kupata mateso kwa ajiri ya utukufu wa Mungu, pia hufundisha kuwa magonjwa yanaweza kuwa mfano wa kuadibishwa na Mungu. Lakini tunahitaji kutafuta ufafanuzi wa kiroho.

- Magonjwa, afya, na uponyaji unapaswa uangaliwe katika hali ya ujumla. Katika utamaduni, Waafrika wanaelewa kuwa afya na usalama ni sehemu ya maisha ya mwanadamu katika ujumla wake. Inafahamika kuwa magonjwa ni ishara ya kuharibika kwa mahusiano na familia, jamii, au mizimu. Hivyo, mara nyingi mwitikio wa mwafrika kuhusu ugonjwa ni kumtembelea mganga wa kienyeji (mpiga ramri) ili asaidie kurejesha hayo mahusiano mazuri ili kuutibu huo ugonjwa kwa miti shamba. Ingawa Wakristo tunapinga namna yoyote ya ibada ya sanamu kupitia tiba asilia (tutaliangalia swala hili kwa undani zaidi katika somo hili hapo baadae) tusipoteze ufahamu wetu wa kiutamaduni kuhusu asili ya afya na ugonjwa katika hali ya ujumla katika maisha ya Mwafrika.

  Mungu anatawala. Mungu ni muumbaji na ni Yeye anayeponya, (Kutoka 15:26). Mungu anauwezo juu ya magonjwa na mauti. Anaweza na huwa anaponya. Mapenzi yake yafanyike. Tunatakiwa kumtii katika hili, hata kama hatuelewi kwanini anachagua kuruhusu magonjwa. Katika Isaya 55:8–9, Mungu anatukumbusha:

  > *"Kwa kuwa mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu sio njia zangu . . .. Kama vile mbingu zilivyo juu kuliko dunia, ndivyo njia zangu na mawazo yangu zilivyo juu."*

- Katika Kristo Yesu, tunazo ahadi zake na tunatazamia kwa tumaini siku zijazo bila magonjwa au mauti au kilio.

## Zoezi 5: Kisa na Mjadara (dakika 30)

**Lengo** — Kuwawezesha washiriki kujadiri tatizo la uchawi.

### Kisa chetu kinarejea …

**Kisome tena kisa**, sehemu ya kwanza ya kisa kwa washiriki:

*Samweli na mke wake Estha wanaishi na mama yao mzee, Yunisi, na watoto wao Paulo (umri wa miaka 10) na Raheli (miaka 8). Pia wanaishi na Gidioni (umri wa miaka 12), ambaye ni mwana wa Samweli kutoka katika mahusiano ya mbali. Samweli anafanya kibarua, na Estha huuza nyanya kando kando ya barabara. Asubuhi moja, Estha aliamka akijisikia mgonjwa. Alikuwa akiumwa sana kichwa. Homa, kuhara, na kichefu chefu. Alijisikia vibaya kiasi cha kushindwa kula, na aliendelea kuwa dhaifu na dhaifu katika siku chache zilizofuata.*

## Kisa chetu kinaendelea …

**Soma kwa sauti sehemu ya kisa kifuatacho**:

*Yunisi alianza kumunung'unikia Samweli kuwa ugonjwa umesababishwa na Gidioni kwa kumuacha mama yake wa kambo. Alimwambia kuwa Gidioni alikuwa mchawi hatari mwenye uwezo, Samweli asipomuondoa mtoto wake katika nyumba, atawaua Estha na wanafamilia wengine. "Nilimsikia Samweli akiita katika usingizi," akisema Yunisi, "ilikuwa kipindi alipomulaani Estha na kumfanya awe mgonjwa."*

*Lakini Samweli alikataa kumutupa mtoto wake mitaani. "Gidioni sio mchawi. Yeye ni mtoto wang una ninampenda. Nitampeleka Estha katika kiliniki. Bilas haka, Madaktari wa hapo wanaweza kutusaidia."*

*Kiungwana Samweli alimchukua mke wake na kumpeleka katika kiliniki iliyokuwa Jirani na mji. Alimsubiria hadi wafike mbele ya foreni. Daktari anaweza kumpima na kugundua kirusi cha ugonjwa. "Virusi viko tu katika mazingira yetu na miili yetu hufanya kazi ya kuvizuia," dakitari alisema. Virusi ni viumbe hai vidogo vidogo vilivyotengenezwa na vinasaba maumbile, ambavyo huingia katika seli za miili yetu na kujizalisha kwa wiingi. Ndio maana hutufanya tujisikie magonjwa. Tunapigana navyo kwa kutumia mfumo wa kinga zetu za mwili, lakini wakati mwingine huchukua muda mrefu, na tunahitaji msaada wa matibabu ili kupona." Alielezea.*

*Alimpatia Estha dawa ili kuzuia zile dalili, hasa homa yake, na alimuelezea Samweli namna ya kumukinga dhidi ya kupungukiwa maji kwa kuchanganya mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji safi, salama na kumpatia akiwa nyumbani. "Upungufu wa maji ni kiini kikubwa cha yeye kujisikia mdhaifu." Alisema daktari.*

*"Je, huu sio uchawi?" Samweli aliuliza.*

*Daktari Maria alisema "Hapana," Ugonjwa wa Estha una maelezo ya kitabibu na kidaktari. Wakati mwingine mfumo wa kinga zetu unakuwa dhaifu kuliko katika kipindi kingine, ndio maana wakati mwingine mtu mmoja huugua na mwingine hapana, au mwingine hupona na mwingine hapana. Tunaweza kuufanya mfumo wa kinga mwilini imara kwa kula vyakula vyenye virutubisho kama vile matunda, mboga za majani, na protini. Lakini pia miili yetu huwa dhaifu kulingana na umri*

> *unavyoongezeka na huwa vigumu kupigana na magonjwa. Bahati nzuri, Estha ni kijana, na ulimuleta mapema kiliniki, na alikuwa na nafasi nzuri ya kufanya uponyaji mwilini mwake."*
>
> *Samweli alimpeleka Estha nyumbani na watoto watatu walimsaidia kumtunza. Baada ya Juma moja, alipata nguvu za kuinuka kutoka kitandani na kutoka nje. "Najisikia vizuri sasa," alimwambia Samweli, "dawa zimeisaidia kinga ya mwilini kwangu kupigana na ugonjwa. Mungu ametuumba vizuri sana, na miili inayoweza kujikarabati yenyewe, na akiri inayoweza kutusaidia kuelewa ugonjwa na namna ya kuutibu. Ninamshukru Mungu kwa Daktari Maria.""*

**Kisimamishe kisa hapa.**

Waalike washiriki kuungana tena na vikundi vyao vidogo na kujadiri maswali yafuatayo kwa dakika 10:

- Watu katika jamii yetu hutafuta wapi maelezo na ufafanuzi kuhusu ugonjwa?
- Kungetokea nini endapo Samweli angekubaliana na ushauri wa Yunisi?
  - Kungepatikana matokeo gani kwa Gidioni?
  - Kungepatikana matokeo gani kwa Estha?
  - Kungepatikana na matokeo gani kwa familia nzima kwa ujumla?
  - Kipindi kingine kungetokea nini endapo mwana familia mmoja angeugua?
  - Ushauri wa Daktari maria ulifanyika kuwa msaada kiasi gani?

**Baada ya dakika 10**, mualike msemaji kutoka kila kundi kushirikisha miitikio yao kwa kila mmoja.

**Hakikisha kusisitiza yafuatayo**:

- **Kama tulivyoonesha hapo awali:** Dhambi hututenga mbali na Mungu. Hali ya kutengwa na Mungu huleta matokeo ya magonjwa na mauti. Kupitia Yesu na kazi zake msalabani, wale wanaompenda huletwa katika mahusiano na Mungu. Lakini mpaka sisi Wakristo tupokee miili yetu mipya isiyoharibika pale Yesu atakaporudi, miili yetu itaendelea kuzeeka na kufa. Magonjwa na mauti ni sehemu ya matakwa ya mwili wa mwanadamu. Biblia inasema kuwa Wakristo waaminifu wanaweza kuingia katika mateso kwa ajiri ya utukufu wa Mungu, na pia hutufundisha kuwa magonjwa yanaweza kuwa njia ya Mungu kumwadibisha mwanadamu. Bali tunahitaji kutafuta maelezo na ufafanuzi wa kiroho.

- Endapo tutajaribu kutafuta ufafanuzi zaidi wa kiroho, tutasababisha au kukaribisha mateso zaidi. Katika kisa chetu, Gidioni angeweza kufukuzwa katika nyumba na kulazimishwa kuishi maisha mabaya na mitaani. Angeweza hata kuangukia matambiko ya wasio amini na kuishi maisha ya upweke na kujihisi kutengwa na kukataliwa. Familia yake ingekuwa imesambaratika. Pia Estha angekuwa amefariki kwa sababu ya kukosa matibabu ya hospitalini.

- Mungu naweza kuponya na huwa anaponya. Yeye huchagua kufanya hivyo moja kwa moja au kimuujiza, au anaweza kuchagua kuponya kwa kutumia matibabu ya kisayansi. Mungu alituzawadia sisi wanadamu uwezo wa kujifunza na kuelewa miili ambayo amaiumba, na jisi ya kuitunza. Ni kweli pia kuwa Mungu *anaweza kuchagua kutoponya*, na hatimaye sisi wote ni wahanga wa mauti hadi kipindi ambacho Yesu alikiita kama 'Siku Zijazo.'

## Zoezi 6: Kisa na Tafakari (dakika 20)

**Lengo** — Kutambua kuwa dawa hazina majibu yote, bali pia tunahitaji kumtumainia Mungu.

### Kisa chetu kinaendelea …

**Wasomee washiriki sehemu ya kisa kifuatacho.**

*Juma moja baada ya Estha kurudi nyumbani kutoka kiliniki, Mchungaji Emmanuel aliitembelea familia. Estha alikuwa amekaa kimya katika kiti na Paulo alimlaki baba yake akitokea shambani na Raheli aliandaa chai, Yunisi akiwa anatazama.*

*"Ni vyema kukuona unaonekana vizuri, Dada Estha," alisema mchungaji Emmanueli wakati Samweli na Gidioni wakitokea mlangoni na kumsaslimia. "Ninafuraha kwa vile daktari wa kiliniki aliweza kukutibu kwa dawa sahihi."*

*"Ndio," Estha alijibu akitabasamu, "Nimebarikiwa sana."*

*"Haswa," alisema mchungaji Emmanueli, "na ulitumia busara kutafuta msaada kiliniki."*

*"Madaktari hawajui kila kitu," Yunisi alisema.*

*"NI kweli kwamba madaktari hawawezi kutambua kila kitu kinachotufanya tuugue, na sio mara zote wanavyo vifaa tiba vya kugundua kila ugonjwa," alijibu mchungaji Emmanueli. "Hawakuweza kuyaokoa maisha ya mke wangu mpendwa, ingawa walijaribu kwa jitihada zote." Kwa muda mfupi tu alinyamaza, nilikumbuka ugonjwa wa mke wake mwaka jana. "Ninamkosa sana mke wangu." Lakini yeye na mimi wote tunamwamini Mungu kuwa katika busara zake na wema wake angefanya kilicho chema kwake (mke wa mchungaji Emanueli). "Hatukutafuta maelekezo ya kiganga, kama vile uganga, na hatukuhatarisha familia yetu na jamii yetu kwa kutafuta mbuzi wa azazeli. Tulielewa kuwa Mungu ametupatia sisi wanadamu uwezo wa kujifunza kuhusu miili yetu na namna inavyofanya kazi na namna ya kuisaidia kukarabati inapokuwa imeugua au kuharibiwa, hii ndio maana ya kutafuta msaada na ushauri wa kidaktari. Lakini wanadamu hawawezi kuwa na majibu yote. Mwishoni, tunapaswa kuyakabidhi maisha yetu katika mikono ya Mungu. Tulitafuta msaada ya kidaktari na tuliomba kwa ajiri ya uponyaji, lakini Mungu alichagua kumchukua nyumbani*

> *kwake ili kuwa pamoja nae mbinguni, kuliko sisi kutaka kumwa nae kwa muda mrefu. Kama Biblia inavyotufundisha katika Isaya 57, 'Watu wema huondoka mapema; wacha Mungu hufa kabla ya wakati wao. Lakini hakuna anayeonesha kujari au kushangaa kwanini. Hakuna anayeonesha kutambua kuwa Mungu anawakinga na mabaya yajayo. Wale waifuatao njia ya haki watapumzika katika amani siku wakifa.' Nina furaha kuwa hiki kiwe kwa mke wangu mpendwa amepumzika kwa amani, hata kama nilimpoteza."*
>
> *Samueli aligusa begani kwa mchungaji Samweli. "Huo ulikuwa wakati mgumu kwako."*
>
> *"Ndio, lakini Mungu huwafariji waliao, na alikuwa karibu nasi kipindi chote cha ugumu. Ni wakati maalum kutambua kuwa yuko pamoja na Bwana na Mwokozi Yesu mbinguni na siku moja nitaungana nao huko."*
>
> *Walikusanyika mahali pamoja wakimsifu Mungu na kuomba, kabla hawajaitumia chai ya Raheli na kula keki kidogo wakiongea na kucheka pamoja.*

**Kisimamishe kisa hapa.**

**Waombe washiriki** kutafakari katika sehemu ya kisa hiki na kushirikisha mawazo yao na kile walichojifunza kutoka katika kundi.

kuwa kama kuna wale ambao walishapata kupoteza wenzi wao wangependa kupata maombi, kutakuwa na wanandoa wawili (huenda wachungaji na wake zao) watakaopatikana mwishoni mwa warsha ili waweze kuongea na kuombewa.

## Zoezi 7: Tafakari ya Biblia (dakika 60)

**Lengo** — Kuangalia mfano wa Yesu.

**Elezea** kuwa sasa tunaenda kuangalia kuhusu mfano wa Yesu, kuona namna alivyowachukulia watu waliokuwa na maumivu na magonjwa.

**Soma kwa sauti** aya zifuatazo:

Mathayo 11:4–5

> *Yesu alimjibu (Yohana Mbatizaji alipouliza kama alikuwa ndiye Masihi au la), "Nendeni mkamwambie mliyoyasikia na kuyaona: vipofu wanaona, viwete wanatembea, wakoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na habari njema inahubiriwa kwa maskini."*

**Waulize washiriki** ni mifano gani kati yah ii ambayo Yesu aliitoa kuhusu uponyaji katika aya hizi.

*Majibu yanayoweza kuwa ni:*

- *Vipofu wanapata kuona;*
- *Vilema na viwete wanatembea;*

- *Ukoma (maumivu yanayosababishwa na bakteria) unapona y;*
- *Viziwi wanasikia;*
- *Mahitaji ya kiroho yanajibiwa.*

**Sasa waulize washiriki** kama wanaweza kufikiri kuhusu hali yoyote ya maumivu na magonjwa ambayo Yesu aliziponya.

*Mifano kadhaa inaweza kuwa:*

- *Maumivu makali, kifafa (kupagawa), na kupooza — katika Mathayo 4:23–25;*
- *Kutokwa damu kusikokoma — katika Mathayo 9:20–22;*
- *Uvimbe — katika Luka 14:6;*
- *Hata mauti — katika Luka 7:11–17, Marko 5:35–43, Yohana 11:1–44.*

**Angalizo la muhimu**: Yesu aliwatoa peopo kwa neno. Kwa maelezo saidi namna Yesu alivyokemea mapepo, tazama Kiini cha Mambo Modula 5 (*Kiini cha Jambo Modula 5, Zoezi 2)*. Kwa kifupi, Yesu aliwaonea huruma waliokuwa chini ya uonevu wa ibilisi. Alikemea pepo kwa neno, aliwachukulia wote aliowaponya kwa huruma na upole.

**Elezea**: Ujumbe unaoeleweka ni kwamba hakuna kitu kilicho kigumu sana kwa Yesu, na kwamba ana mamlaka yote dhidi ya magonjwa na mauti, na dhidi ya Shetani na madhara yake.

## Yesu anaponya

**Elezea**: tunaenda kuangalia jinsi Yesu alivyowaponya watu.

**Omba watu wa kujitolea kusoma** kila aya zifuatazo.

Baada ya kila kusoma, **waulize washiriki:**

- Ni njia gani Yesu aliitumia kumponya mtu katika kisa hiki?

## Aya za Biblia

**Marko 7:33–35**

> *Yesu aliweka vidole vyake kwenye masikio ya kiziwi. Kisha alitema mate na kuugusa ulimi wa yule mtu. Alitazama mbinguni na akavuta hewa, akamwambia , "Efatha!" (yaani 'funguka).' Mara tu masikio yake yakafunguka na ulimi wake ukaachiliwa, akaanza kuongea sawasawa.*

**Yohana 9:1–7**

> *Yesu alipokuwa akipita, alimwona mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamuuliza, "Rabi ni nani aliyetenda dhambi, ni huyu mtu au wazazi wake hata azaliwe kipofu?"*
>
> *"Yesu akawajibu, "Huyu mtu wala wazazi wake hawakutenda dhambi. Alizaliwa kipofu ili kazi ya Mungu zidhihirishwe katika maisha yake. Yanipasa kuzifanya*

> *kazi yake yeye aliyenituma wakati bado ni mchana, kwa maana usiku waja ambapo hakuna mtu awezaye kufanya kazi. Wakati niko ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu."*
>
> *Baada ya kusema haya, akatema mate ardhini, akatengeneza tope kwa mate na akampaka yule mtu kipofu machoni. Kisha akamwambia, "Nenda ukanawe katika bwawa la Siloamu." (Siloamu maana yake ni aliyetumwa). Ndipo yule kipofu akaenda, akanawa, naye akarudi akiwa anaona.*

**Marko 10:51–52**

> *"Yesu akauliza, "unataka nikufanyie nini?" Yule kipofu akajibu, Rabi, nataka kuona."*
>
> *"Yesu akasema, "Nenda, imani yako imekuponya. Mara akapata kuona, akamfuata Yesu njiani.*

**Luka 8:43–48**

> *Katika umati huo, palikuwa na mwanamke aliyekuwa akitokwa damu kwa muda wa miaka kumi na miwili. Tena alikuwa amegharimia yote aliyokuwa nayo kwa ajiri ya matibabu, wala hakuna yoyote aliyeweza kumponya. Huyo mwanamke akaja kwa nyuma ya Yesu na kugusa upindo wa vazi lake. Mara kutokwa damu kwake kukakoma.*
>
> *Yesu akauliza." Ni nani aliyenigusa?" Watu wote walipokana, Petro akasema, Bwana, umati wa watu unakusonga na kukusukuma kila upande." Lakini Yesu akasema, "kuna mtu aliyenigusa, kwa maana nimetambua kuwa nguvu zimenitoka."*
>
> *Yule mwanamke alipofahamu ya kuwa hawezi kuendelea kujificha, alikuja akitetemeka, akaanguka miguuni pa Yesu. Akaeleza mbele ya watu wote kwanini alimgusa na jinsi alivyoponywa mara moja. Basi Yesu akamwambia, "Binti, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani."*

**Luka 7:2–10**

> *Mtumishi wa jemadari mmoja wa Kirumi, ambaye bwana wake alimthamini sana, alikuwa mgonjwa sana karibu kufa. Jemedari huyo aliposikia habari za Yesu, aliwatuma wazee wa Kiyahudi kwake, wakamwomba aje kumponya mtumishi wa huyo jemedali. Wale wazee walipofika kwa Yesu, wakamsihi sana wamsaidie yule wakisema,*
>
> *Bwana mtu huyu anastahili wewe umfanyie jambo hili, kwa sababu analipenda taifa letu tena ametujengea Sinagogi letu." Hivyo Yesu akaongozana nao, lakini alipokuwa karibu na nyumba, yule jemedari akatuma watu kumwambia Yesu, "Bwana usijisumbue, kwani mimi sistahili wewe kuingia chini ya dari yangu. Ndio maana sikujiona hata ninastahili kuja kwako wewe. Lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu atapona. Kwa kuwa mimi mwenyewe ni mtu niliyewekwa chini*

> *ya mamlaka, nikiwa na askari chini yangu. NIkimwambia huyu nenda,' yeye huenda; na mwingine nikimwamba, 'njoo,' yeye huja. NIkimwambia mtumishi wannngu, 'fanya hivi,' yeye hufanya."*
>
> *Yesu aliposikia maneno haya, alishangazwa naye sana. Akaugeukia ule umati wa watu uliokuwa unamufuata, akawaambia, " sijaona imani kubwa namna hii hata katika Israeli. Nao watu waliokuwa wametumwa kwa Yesu waliporudi nyumbani walimkuta yule mtumishi amepona.*

**Yohana 4:49–50**

> *Yule afisa wa mfalme akamwambia, bwana tafadhali shuka kabla mwanangu hajafa."*
>
> *"Yesu akamwambia, "Enenda zako mwanao yu hai."*
>
> *Yule afisa akaamini yale maneno aliyoambiwa na Yesu, akaondoka akaenda zake.*

**Yohana 11:38–44**

> *Yesu kwa mara nyingine akiwa amefadhaika sana, akafika kwenye kaburi. Hilo kaburi lilikuwa pango ambalo jiwe lilikuwa limewekwa kwenye ingilio lake. Yesu akasema liondoeni jiwe hilo."*
>
> *"Martha ndugu yake yule aliyekuwa amekufa akasema, "Lakini Bwana, wakati huu atakuwa ananuka kwani amekwisha kuwa kaburini siku nne." Yesu akamwambia, "sikukuambia kwamba kama ukiamini utauona utukufu wa Mungu.*
>
> *Kwa hiyo wakaliondoa lile jiwe kutoka kaburini. Yesu akainua macho yake juu akasema, "baba, ninakushukru kwa kuwa wewe hunisikia siku zote, lakini nimesema haya kwa ajiri ya umati wa watu hawa uliosimama hapa, ili wapate kuamini kuwa wewe umenituma."*
>
> *Baada ya kusema haya, Yesu akapaza sauti yake akaita, "Lazaro, njoo huku!" Yule aliyekuwa amekufa akatoka nje, mikono yake na miguu yake ikiwa imeviringishwa vitambaa vya kitani na leso usoni pake.*
>
> *Yesu akawaambia, "Mfungueni, mwacheni aende zake."*

Baada ya washiriki wote kutoa majibu yao, **sisitiza vipengele vifuatavyo**: Yesu aliponya kwa njia nyingi mbali mbali. Wakati mwingine hakuwepo wakati mtu anaponywa. Nguvu zake zinajitosheleza.

- Yesu aliponya mara nyingi kama sehemu ya huduma yake, lakini umuhimu mkubwa katika kufanya hivi ilikuwa kuonesha kuwa yeye allikuwa Masihi. Hata hivyo, Yesu hakuwaponya wote waliokuwa wagonjwa, lakini alitenda katika kila muktadha ili kwamba baba yake atukuzwe.

- Mara nyingi Yesu aliponya kama sehemu ya huduma yake, lakini umuhimu wa kufanya hivi ilikuwa kuonesha kuwa Yeye alikuwa Masihi. Hata hivyo Yesu hakuwaponya wote waliokuwa wagonjwa, lakini alitenda katika kila eneo ili Baba yake atukuzwe.
- Sehemu zingine za Biblia zinaonesha kuwa wafuasi wake waliendeleza huduma ya uponyaji. Lakini kama tulivyoona kutoka katika mfano wa Timotheo na Trophimo, Mungu hakuchagua kuponya kupitia wao.
- Miujiza ya uponyaji wa papo kwa hapo haiwezi kumpata kila mmoja, na ukweli ni kwamba wengi wetu tutajionea afya dhaifu. Na sisi wote tutajionea mauti.

# Zoezi 8: Kisa Mlinganisho wa Maoni (dakika 40)

**Lengo** — Kuchunguza njia ya busara kutafuta uponyaji.

## Kuitambulisha mada

**Sisitiza vipengele muhimu vifuatavyo**:

- Miujiza ya uponyaji wa papo kwa papo haiwezi kuwa uzoefu wa kila mmoja. Ukweli ni kwamba kila mmoja wetu atapata afya iliyodhoofika na sisi wote tutajionea mauti. Tunapaswa kuzingatia mifano kutoka katika Biblia inayotukumbusha kuhusu ukweli huu.
  - 1 Wafalme 14:4 inasema “Wakati huo (nabii) Ahiya alikuwa kipofu; alishindwa kuona kwa sababu ya umri wake.”
  - Hata Elisha, mmoja wa manabii wakubwa na mtenda miujiza mikubwa ghafla aliugua na kufa. 2 Wafalme 13:14 inatuambia “Sasa Elisha aliugua na kutokana na ugonjwa huo alifariki.”
  - Tunajifunza pia katika Wafilipi 2:25-30 kuhusu Epafrodito aliyeponywa, lakini taratibu na ilichukua muda. Tunajifunza kuwa habari za ugonjwa wake zilifika hadi Filipi na kuwafanya Wakristo kuhusika. Paulo hakuwa na wazo kuwa angemponya Epafrodito. Uponyaji haukuwa kitu ambacho kingetawala, haijalishi mamlaka aliyokuwa nayo kama mtume.

**Sisitiza yafuatayo**:

- Katika mifano yote hii, hakuna kipengele chochote kuwa ushirikina ulitumika.
- Ni halisi kuwa uponyaji wa papo kwa papo sio lazima kuufanya muujiza uwe muujiza.

**Elezea:** Sasa tutalichunguza swali, “Tunatakiwa tufanye nini endapo sisi au wengine wakiugua?” Sasa tutaangalia katika sehemu nyingine ya kisa kilichobakia kuhusu Samweli na Estha na familia zao.

## Kisa chetu kinaendelea…

**Wasomee washiriki kwa sauti** sehemu ya kisa kilichobakia**.**

*Majuma machache yaliyopita, dada yake na Samweli, Lydia, aliitwa na binti yake na Elizabethi, ambaye ana umri wa miaka 13. Wanapoendelea kuongea na Samweli, Estha, Yunisi, na Watoto wao, Samweli aligundua kuwa Lydia na Elizabethi walikuwa wamevaa hirizi.*

*“Kwanini umevaa hizi hirizi?” alimuuliza Lydia, akisonta kiuno chake.*

*“Kuna ugonjwa katika kijiji chetu,” alijibu. “Nilinunua hirizi hizi kwasababu niliambiwa kuwa zitanikinga dhidi ya magonjwa na zitatuponya tutakapopata magonjwa.”*

*“Lakini wewe sio Mkristo?” Samweli aliuliza. “Biblia inatuambia kuwa Mungu hatutaki sisi kuzitumainia hirizi.”*

*Lydia aliuliza, “Una uhakika?” Lydia aliuliza, akionekana kutoelewa. “Unaweza kunionesha namna Biblia inavyosema kuhusu ushirikina na hirizi?”*

*Samuweli aliichukua Biblia yake iliyokuwa chini ya mto wake na kufunua Ezekieli 13 aya 20. Hiki ndicho Biblia isemavyo katika kitabu cha Ezekieli,” alisema. Naye alianza kusoma: “Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Mimi niko kinyume na hizo hirizi zenu za uchawi ambazo hizo mnawatega watu kama ndege, nami nitazirarua kutoka mikononi mwenu, nitawaweka huru watu wale waliowatega kama ndege*.”

*“Hivyo ushirikina hauwakilishi nguvu za Mungu bali hugeuza usikivu wetu kutoka kwenye ukweli wa ibada yetu,” alielezea Samweli. “Mungu ndiye wa kutumaini. Mungu haahidi kuwa hatutaondoka katika maumivu na mateso, lakini yeye ni kimbilio na msaada. Kuvaa hirizi za kichawi au kufanya tambiko linaloelekea kwenye miungu ya uongo, roho, au kwa wafu waliohai, ili kupata ulinzi au uponyaji ni kama kuabudu miungu mingine, ambayo haikubaliki kwa Mungu wetu mmoja na wa kweli.”*

*Lydia aliacha kidogo kunywa kinywaji chake na akamsikiliza kwa makini Samweli alipokuwa anaendelea kuongea. Ushirikina umeungamanishwa na hofu,” alisema. “Hofu kwamba kitu kibaya kitatokea. Lakini Biblia imetuambia kuwa tusiogope. Warumi 8 aya ya 37-38 inasema hakuna kitakachotutenganisha na upendo wa Mungu Baba. Mungu wetu ana nguvu zote, na uwezo wote. Ni yeye peke yake anaeweza kutukinga kweli kweli. Watu wanaotuuzia ushirikina na vitu vingine ambavyo vina nguvu kama vile ‘maji ya baraka au mafuta maalum wanatafuta kututumia kwa ajiri ya makusudi yao ubinafsi, wao kama vile sanamu na fedha. Tunapojaribiwa kutegemea ushirikina na hirizi, tunapswa kuomba maombi aliyoomba Daudi katika Zaburi 31 aya 4 ambayo inasema: ‘Uniepushe na mtego niliotegewa, maana wewe peke yako ndie kimbilio langu.’”*

Edition 2021–01b

*"Oh," Lydia alisema, "Sikufahamu hayo. Tunatakiwa kuondoa ushirikina mara moja." Samweli alitafuta kisu na Lydia alikata sehemu ya hirizi katika kiuno chake na ile iliyokuwa imevaliwa na Elizabethi.*

*"Kwa hiyo, tunafanye nini ili kujikinga wenyewe, au endapo tutakuwa wagonjwa?" Aliuliza.*

*"Hata hivyo Biblia inasema kuwa tunaweza kupata uponyaji. Hii inaweza kuwa kupitia maombi, kupitia kupakwa mafuta na maombi ya wazee wa kanisa, kupitia njia za kisayansi za sasa, na kupitia njia za asili za uponyaji ikizingatia hazihusiani na matambiko ya kiroho au imani zinazotokana na ushirikina, au zile zinazoenda kinyume na mafundisho ya Kikristo. Wakristo hawapaswi kwenda kwa mganga wa mpga ramli ambaye anatumia au kudai kutumia aina yoyote ya matambiko ya kishirikina au ya nguvu za kiroho. Mnamkumbuka Elmasi katika Matendo ya Mitume 13? Paulo alimtuhumu kuwa muongo na mjanja na kuwa ni mwana wa mwovu. Hakupaswi kuwa na madhara kwa mtu anayetafuta uponyaji. Hakupaswi kuwa na matumizi ya vidonge vya kulevya, au aina hatari ya uponyaji wa ibada unaohusishwa na tuhuma za kichawi, ambazo zinapelekea hisia, na uharibifu wa kiroho.*

*"Kumbe. Lydia aliuliza, "Vipi kuhusu sayansi ya madawa na madaktari?"*

*"Yesu alidhani kuwa madaktari walikuwa watu sahihi kutibu magonjwa." Samweli alifungua Biblia yake katika Mathayo 9 aya 12, na kusoma: "Yesu alisema 'Watu wenye afya hawahitaji daktari, wagonjwa wanamhitaji daktari." Yesu aliendelea, "Kwa hiyo, inapowezekana, ni vyema kusikiliza ushauri wa madaktari na manesi, wanaoelewa kilichosababisha ugonjwa na namna ya kuutibu. Pia wanatusaidia kujikinga kwa kutufundisha kama vile kutunza usafi tunapokula au tunapotumia choo, au kwa kuchukua matibabu sahihi kuzuia kifafa na michango."*

*ELizabethi aliuliza, "Vipi kuhusu wachungaji wetu? Je wanaweza kusaidia?"*

*"Haswa," Samweli alijibu. Wakizingatia kuwa wachungaji wema wnaofuata mfano wa Yesu. Mara zote tunatakiwa kuangalia mfano wa Yesu. Yesu alipowaponya wagonjwa, hakutumia mbinu mkanganyiko au maneno, au kupiga kelele na kupaza sauti au kutumia nguvu za kimwili na kujeruhi watu, muda wote alikuwa mpole na mwenye huruma. Hakuna aliyepata madhara ili kupata uponyaji. Wachungaji wema wanajua jinsi ya kuomba na kumpaka mafuta mgonjwa kama ilivyoelezewa na Yakobo. Mungu anaweza na huwa anaponya watu, lakini hawezi kuchanganywa kidanganyifu. Hakuna njia maalum inayoweza kumfanya au kumlazimisha kumponya mtu. Tusijiruhusu kupelekwa na mbinu mpya ya kutenda miujiza. Tazama hapa Wakolosai 2 aya ya 8 inasema, 'angalieni mtu yeyote asiwafanye nyinyi mateka kwa elimu batili na madanganyo matupu yanayotegemea mapokeo ya wanadamu na mafundisho ya ulimwengu badala ya Kristo.'"*

> *Lydia alisema, "Sasa naelewa vizuri.*

**Kamilisha kisa hapa.**

## Kumbuka vipengele vya muhimu

**Chora** jedwari likiwa na safu mbili likiwa na vichwa vya habari FANYA na USIFANYE.

**Wakaribishe washiriki,** shirikisha ujumbe muhimu uliokuwa katika mafundisho ya Samweli kutoka katika Biblia.

Jedwari lililokamilika linatakiwa lionekane kama ifuatavyo:

<table>
<tr><th>FANYA</th><th>USIFANYE</th></tr>
<tr><td>
<ul>
<li>Tafuta na fuata ushauri wa kidaktari kuhusu kuzuia na kutibu ugojnwa.</li>
<li>Omba maombi kuwa Mungu akuponyeshe kama ni mapenzi yake kufanya hivyo.</li>
<li>Kubali kwamba uponyaji huja kwa njia nyingi:
<ul>
<li>Papo kwa papo; kimiujiza;</li>
<li>Kila wakati;</li>
<li>Kupitia maombi;</li>
<li>Kupitia sayansi ya madawa;</li>
<li>Kupitia dawa za miti:<br>— kwa kuzingatia njia hizi sio hatarishi au kutumika kwa Pamoja kuchanganya na na nguvu za matambiko, au katika njia zingine zisizokuwa za mafundisho ya Biblia.</li>
</ul></li>
<li>Kukubaliana kuwa magonjwa na mauti ni sehemu ya kawaida ya maisha ya mwanadamu na kuwa Mungu anatawala na huwa haponyi muda wote.</li>
</ul>
</td><td>
<ul>
<li>Kuweka tumaini katika ushirikina au matambiko kuzuia au kutuponya.</li>
<li>Kwenda kwa ‘mponyaji’ anayoiita miungu ya uongo au maroho, wafu au nguvu:<br>— njia hizi zinapingana na mafundisho ya Biblia.</li>
<li>Kukubaliana na njia za udhalilishaji au zinazosababisha madhara, kujikata, kupiga, kuunguza, na matumizi ya dawa za kishirikina au vinywaji, na unyanyapaa:<br>— kwa mfano, kama matokeo ya mtu fulani kutuhumiwa uchawi.</li>
</ul>
</td></tr>
</table>

**Ibandike** karatasi ukutani karibu na ile yenye majibu ya zoezi la 2.

## Kulinganisha majibu

**Waombe washiriki** kurudi katika makundi yao madogo na wajibu maswali yafuatayo:

- Je ni namna gani majibu yetu ya zoezi 2 yanalinganishwa na yaliyoko katika jedwali?
- Je kuna kitu tunahitaji kukifanya toauti?
- Je kuna kitu tunahitaji kuacha kukifanya?
- Tunahitaji kufanya nini ili kufikia haya malengo?

**Baada ya dakika 10**, mwalike msemaji kutoka kila kundi kushirikisha majibu. **Ongoza mjadara** kuhusu mawazo yaliyokwisha shirikishwa na wasaidie washiriki kuamua kuhusu hatua za kuchukua kutoka katika mafunzo.

# Zoezi 9: Hatua Zifuatayo (dakika 20)

**Lengo** — Tathimini warsha na hakikisha hatua zaidi na fuatilia.

## Kushirikisha mawazo

**Mpatie kila mmoja kipande kodogo cha karatasi.** Waombe washiriki waandike vitu vitatu walivyojifunza leo, na pia andika sentensi moja au mbili kuhusu walichofikiri leo. Waambie wasiandike majina yao katika karatasi. Wapatie dakika chache za kuandika.

Kisha **vikusanye vipande hivyo vya karatasi**, na viweke pamoja. Kisha (bila mpangiliao) wasomee majibu tofauti tofauti katika kundi lote kwa pamjoja.

## Mpango binafsi

**Mpatie kila mshiriki mpango kazi** (tazama kiambatanisho 1).

**Elezea yafuatayo kwa kila mmoja**:

> Hii ni nyaraka binafsi ambayo haitashirikishwa na washiriki wengine. Kila mmoja atachukua mpango kazi wake mwenyewe mwishoni mwa kipindi. Mpango kazi binafsi ni kumsaidia kila mmoja ili kuweka katika matendo kile kilichofunzwa kwa siku.
>
> **Elezea** kuwa kama mwezeshaji, ungependa nakala (picha) ya kila mpango kazi wa kila mmoja na kuuhifadhi, kama kila mshiriki atakubaliana. Utaweza pia kuwafuatilia baada ya miezi mitatu au sita au mwaka mmoja kuanzia sasa (inategemea na kipaumbele), ili kuona maendeleo walioyafanya na kuyaweka katika matendo, na pia kutoa na kusaidia na kutia moyo iwezekanavyo.

**Sasa waombe washiriki** wa kila kundi kukamilisha mpango wao mkakati mara moja.

# Kufunga (dakika 5)

**Mpatie kila mmoja cheti cha mahudhurio**, na kisha mshukru kila mmoja kwa usikivu wake na michango yao kipindi cha warsha.

**Mwalike mshiriki** kufunga kwa maombi.

# Kiambatanisho 1: Hatua Zifuatazo

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tarehe | | Kanisa | |
| Majina | | Mji au Kijiji<br>Jimbo au Mkoa | |

Tunachojitoa kufanya baadae kusaidia watu walio na mateso ya maumivu wanaohitaji msaada wetu ...

| **Hatua 1:** tutafanya nini? | **Watu**: nani atafanya? |
|---|---|
| | |
| | **Muda**: tutafanya lini? |
| | |

| **Hatua 2:** tutafanya nini? | **Watu**: nani atafanya? |
|---|---|
| | |
| | **Muda**: tutafanya lini? |
| | |

| **Hatua 3:** tutafanya nini? | **Watu**: nani atafanya? |
|---|---|
| | |
| | **Muda**: tutafanya lini? |
| | |

Edition 2021–01b